**JINA: ……………………………………………………………DARASA……………………**

**SHULE: …………………………………………………………TAREHE……………………**

**NAMBARI YA USAJILI: ……………… NAMBARI YA MTIHANI ……………………**

**TATHIMINI YA PAMOJA YA NYAHOKAKIRA 3**

**102/3**

**FASIHI**

**OKTOBA 2022**

**Muda: saa 2½**

**Maagizo**

- *Andika **jina lako**, **la shule** na **nambari yako** katika nafasi ulizoachiwa.*
- *Yajibu jumla ya **maswali manne.***
- *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
- *Yajibu maswali mengine **matatu** kati ya yale yaliyosalia.*
- *Usijibu maswali mawili kutoka **sehemu moja.***
- *Majibu yote yaandikwe kwa **lugha sanifu** ya Kiswahili.*
- *Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapa.*
- *Mtahiniwa ahakikishe **maswali yote** yamo na yamepigwa chapa sawasawa.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| **SWALI** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **TUZO** | | | | | | | | | |

**SEHEMU YA A – USHAIRI**

**SWALI LA LAZIMA**

1. Siniite chakaramu, kwa raha zangu maisha
Hata kula visotamu, bora bado sijaisha
Maisha japo magumu, fukara nazidi kasha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Hiki changu sicho sumu, nakipenda kwa bashasha
Ni bora tena kitamu, sioni kikiniwasha
Siongezei saumu, kesho kitanifikisha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Naweka tumboni humu, sifanyi kuwachekesha
Kwangu hiki ni muhimu, kinanitosha kutosha
Kinanipa nyingi hamu, kweli kinanishibisha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Mungu wetu so mgumu, wakati huu taisha
Sinani la gurudumu, sina hata kubwa kasha
Nasubiri kwa hamumu, kesho itawa tamasha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Kushika hiyo kalamu, hichi kimeniwezesha
Sina wa kumulaumu, Mola menisimamisha
Silo shida ya kudumu, nacheki karibu kwisha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Tamu yangu kesho tamu, magumu nayafurusha
Nafikia bora zamu, kuonja tamu maisha
Vikwazo navishutumu, mema nayakaribisha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

Maisha sinidhulumu, uzee sijafikisha
Naomba bora taimu, mawi sinihangaisha
Natoka leo janamu, tena sije nikimbisha
Ipo siku yaja kweli, tala vinono vitamu

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
(b) Fafanu ujumbe katika shairi hili. (alama 3)
(c) Liweke shairi katika bahari tatu tofauti. (alama 3)
(d) Tambua nafsi neni na nafsi nenewa. (alama 2)
(e) Tambua idhini tatu za kishairi shairini na umuhimu wao. (alama 3)
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya kinathari. (alama 3)
(g) Tathmini matumizi ya kibwagizo katika shairi hili. (alama 3)
(h) Tambua aina mbili za usambamba shairini. (alama 2)

**SEHEMU YA B, RIWAYA: Chozi la Heri na Assumpta K. Matei**

***2. '….unajikokota nyumbani, moyoni ukiamini kwamba ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa, kwamba hata kosa lako likawa kubwa vipi,teke la kuku halimuumizi mwanawe…Halafu unaloambiwa ni,Umeipaka mashizi familia hii….***

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

(ii) Andika nafsi ya usimulizi iliyotumiwa katika dondoo hili. **(alama2)**

(iii) Fafanua toni ya dondoo hili. **(alama2)**

(iv) Bainisha mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama2)**

(v) Fafanua umuhimu wa usimulizi wa msemaji wa dondoo hili katika kujenga riwaya hii. (**alama10)**

3. a) ***"Niliwahurumia vijana hawa wakembe ambao walikufa kifo walichoweza kukiepuka."***

Kwa kurejelea riwaya, eleza namna wahusika mbalimbali walivyokufa kifo ambacho wangeweza kukiepuka. **(alama 10)**

b) fafanua umuhimu wa usimulizi wa wahusika wafuatao katika kuijenga Riwaya Chozi la Heri.

**i)** Pete **(alama 5)**
ii) Sauna **(alama 5)**

**SEHEMU YA C:TAMTHILIA: Kigogo na Pauline Kea**

4. ***'Wakujichunga ni wewe pwagu. Mtanitambua na …."***

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
**b)** Fafanua umuhimu wa msemaji. **(alama 4)**
c) Tambua mbinu mbili za tamathali katika dondoo hili. **(alama 2)**
**d)** Bainisha toni katika dondoo hili. **(alama 2)**
**e)** Jadili hatua ambazo mwandishi amependekeza kutetea haki. **(alama 8)**

5. a) Kwa kutolea mifano mwafaka ,eleza jinsi mitindo ifuatayo ilivyotumika katika tamthlia ya Kigogo.
   i) Jazanda **(alama 5)**
   **ii)** Majazi **(alama 5)**

   b) kwa mifano tosha,onyesha matumizi ya mbinu ya ishara kama ilivyotumiwa katika Tamthlia ya Kigogo. **(alama 10)**

**SEHEMU YA D:HADITHI FUPI:**

**Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda**

6. ***Hivyo ndivyo kusema sijui lolote wala chochote. Kwamba mimi si chochote wala lolote katika medani yamasomo? Miaka hii yote imepotea tu vivi hivi? Miaka ya kirango cha kila siku cha kilometa sita kwenda shule ya kutwa ya Busukalala na kilometa sita kurejea nyumbani Busuamka. Karo yote niliyolipa iwe bure? La hasha! Pesa alivyolipa baba Luseme imekwenda bure? Imekwenda kama chendacho kwa mgangakisichokuwa na marejeo? Nitamwambia nini baba? mama anaweza kuelewa kidogo. Lakini baba! Nitamwelezaje haya? Naona mama na baba wameumbwa kwa aina tu.***

(a) Fafanua sifa nne za kimtindo katika dondoo hili **(alama4)**

(b) Eleza namna mandhari imetumika hadithi ya mtihani wa maisha **(alama4)**

(c) Umaskini ndio chanzo cha matatizo ya jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi za: **(alama 12**)

i. Mapenzi ya Kifaurongo
ii. Ndoto ya Mashaka

7. a) "***Hawa wana nini wanachokichelea? Hawa wana kitu gani wasichoweza kukifanya? Hawa wanajali nini kuhusu maskini kama sisi?"***

i) Weka dondoo katika muktadha wake **(alama 4)**

**ii)** Safari ya kuikomboa jamii inahitaji ushirikiano. Thibitisha kwa kurejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba. **(alama 6)**

b) Fafanua changamoto zinazokumba vijana ukirejelea hadithi zifuatazo:

**i)** Mtihani wa Maisha **(alama 5)**

**ii)** Tulipokutana Tena. **(alama 5)**

iii)

**<u>SEHEMU E. FASIHI SIMULIZI</u>**

Leleti, umekosea
Kuchukua kibuzi cha wenyewe,
bila ruhusa
ya wazazi.
Wazee watakuandama,
utaadhibiwa.

Sijakosea,
Tuliagana, tukasikilizana ila
Mahari watakayo
Sinayo
Mie ngefanyaje?

Ngeenda kwa wajomba
Magombe wakukirimie
Wakikosa,
Wakopeshe, hata wakanunue

Leleti, kibuzi cha wenyewe;
regesha ,
Kabla ,
Kivunjike guu kisha
Adhabu iongezeke

Babu, sirejeshi
Kwani penzi limenoga
Nacho kibuzi kilitorekea huku
Na kimedinda… kuozea kwao

Ole wako kijulanga,
Adhabu yaja kama shoka la kukata mti
litakuangukia
mjukuu
rejesha!

Sawa babu!
kesho mafungulia ng'ombe
tarejesha…

**Maswali**

a) Tambua kipera kikuu kinachojitokeza katika utungo huu kwa kutolea sababu. **(alama 1)**
b) Utungo huu unaweza kuwekwa katika tanzu mbili za fasihi simulizi. Zitambue. **(alama 2)**
c) Eleza sifa tatu za kipera ulichotambua. **(alama 3)**
d) Bainisha toni ya kifungu hiki **(alama 2)**
e) Fafanua mgogoro katika utungo huu. **(alama 2)**
f) Fafanua sifa mbili za mrejelewa katika utungo huu. **(alama 2)**
g) Bainisha tamathali mbili za usemi katika kifungu hiki. **(alama 2)**
h) Fafanua majukumu yoyote matatu ya watu wazima kwa kurejelea kifungu hiki. **(alama 6)**